**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU SAYANSI NA TEKNOLOJIA**



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 1026

Jina la Chapisho: Muhtasari wa Somo la Upimaji na Tathmini Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

ISBN: 978-9987-09-749-4

Muhtasari huu umeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 29 Juni 2023 kuwa Muhtasari wa Somo la Upimaji na Tathmini Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali nchini Tanzania.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

# MUHTASARI WA SOMO LA UPIMAJI NA TATHMINI STASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA AWALI

**2023**

© Taasisi ya Elimu Tanzania  2023

Toleo la Kwanza  2023

ISBN:978-9987-09-749-4

aasisi ya Elimu Tanzania
Eneo la Mikocheni
132 Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S. L. P. 35094
14112 Dar es Salaam

Simu: +255-735041168/ +255-735041170
Baruapepe: director.general@tie.go.tz
Tovuti: www.tie.go.tz

Muhtasari huu urejelewe kama: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. (2023). *Muhtasari wa Somo la Upimaji na Tathmini Elimu ya Awali.* Taasisi ya Elimu Tanzania.

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kutoa muhtasari huu au sehemu yake kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi kutoka Taasisi ya Elimu Tanzania.

.

# Yaliyomo

Orodha ya majedwali ........ v
Vifupisho ........ vi
Shukurani ........ vii
1.0 Utangulizi ........ 1
2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania ........ 1
3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu ........ 2
3.1 Lengo kuu la Elimu ya Ualimu ........ 2
3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu ........ 2
4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu ........ 3
5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi ........ 3
6.0 Majukumu ya Mkufunzi Mwalimu Tarajali na Mzazi katika ufundishaji na Ujifunzaji ........ 4
6.1 Mkufunzi ........ 4
6.2 Mwalimu Tarajali ........ 4
6.3 Mzazi ........ 5

7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 5

8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 5

9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji ........ 6

10.0 Idadi ya Vipindi ........ 7

11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji ........ 7

Bibliografia ........ 12

# Orodha ya Majedwali


Jedwali Na 1: Umahiri mkuu na mahususi kwa Mwaka wa Kwanza na wa Pili ........ 4

Jedwali Na 2: Alama za upimaji endelevu kwa masomo ya utaalamu na ya jumla ........ 6

Jedwali Na 3: Maudhui ya Mwaka wa Kwanza ........ 7

Jedwali Na 4: Maudhui ya Mwaka wa Pili ........ 10

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| WyEST | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia |

# Shukurani

Maandalizi ya Muhtasari wa Somo la Upimaji na Tathmini Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali yamehusisha wataalamu mbalimbali kutoka taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki wote waliofanikisha uandaaji wa muhtasari huu. Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa wahadhiri, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule, walimu pamoja na wakuza mitaala wa TET. Vilevile, TET inaishukuru Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kusimamia Kazi ya Maboresho ya Mitaala ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu iliyoteuliwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati hii ilifanya kazi kwa weledi na kuhakikisha kuwa maudhui ya muhtasari huu yanalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, ujuzi na stadi zitakazowawezesha kujiajiri, kuajiriwa na kumudu maisha yao ya kila siku, ambalo ndilo lengo kuu la uboreshaji wa Mitaala ya Mwaka 2023.

Mwisho, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandaaji na usambazaji wa muhtasari huu.



Dkt. Aneth A. Komba

Mkurugenzi Mkuu

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

## 1.0 Utangulizi

Somo la Upimaji na Tathmini ni la lazima katika Stashahada ya Ualimu Elimu ya Awali. Ujifunzaji wa somo hili utamwezesha Mwalimu tarajali kuwa na uwezo wa kuchambua mbinu mbalimbali za upimaji na tathmini katika elimu ya awali, kumudu mbinu za kuandaa zana za upimaji wa maendeleo ya ukuaji wa mtoto na kumudu mbinu za kutoa mrejesho na afua stahiki kwa kutumia matokeo ya upimaji na tathmini katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Vilevile, somo hili litamwezesha Mwalimu tarajali kukuza uwezo wa kumsaidia mtoto kujifunza, kupima maendeleo ya mtoto, kuboresha ufundishaji pamoja na kutathmini ubora wa ufundishaji wake. Aidha, anatarajiwa kuwa mnyumbufu katika kutengeneza mazingira wezeshi ya ufundishaji na ujifunzaji. Muhtasari umeandaliwa ili kuongoza ufundishaji na ujifunzaji wa Upimaji na Tathmini wa Ualimu ngazi ya Stashahada ya Elimu ya Msingi Tanzania bara. Muhtasari unatoa maelekezo ya kuwawezesha Wakufunzi kuandaa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa walimu tarajali kwa ufanisi. Vilevile, muhtasari unatoa nafasi kwa Wakufunzi kutumia mbinu mbalimbali za ufundishaji na ujifunzaji wa Somo la Upimaji na Tathmini.

## 2.0 Malengo Makuu ya Elimu Tanzania

Malengo makuu ya elimu Tanzania ni kumwezesha kila Mtanzania:

(a) Kukuza na kuboresha haiba yake ili aweze kujithamini na kujiamini;

(b) Kuheshimu utamaduni, mila na desturi za Tanzania, tofauti za kitamaduni, utu, haki za binadamu, mitazamo na matendo jumuishi;

(c) Kukuza maarifa na kutumia sayansi na teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi, na maendeleo endelevu ya taifa na dunia kwa ujumla;

(d) Kuelewa na kulinda Tunu za Taifa ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, uadilifu, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji na lugha ya taifa;

(e) Kujenga stadi za maisha na stadi za kazi ili kuongeza ufanisi katika maisha ya kila siku;

(f) Kukuza tabia ya kupenda na kuheshimu kazi ili kuongeza tija na ufanisi katika uzalishaji na utoaji wa huduma;

(g) Kutambua na kuzingatia masuala mtambuka ambayo ni pamoja na afya na ustawi wa watu (jamii), usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira; na

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa na kimataifa, amani na haki kwa kuzingatia Katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa.

## 3.0 Malengo ya Elimu ya Ualimu

### 3.1 Lengo kuu la Elimu ya Ualimu

Lengo kuu la elimu ya ualimu ni kumwandaa mwalimu mwenye weledi na umahiri wa kuwezesha ujifunzaji na ufundishaji unaoendana na mabadiliko ya kisayansi, kiteknolojia, na kijamii ili kumjenga Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mitazamo chanya, na anayethamini usawa, haki na elimu bila ukomo.

### 3.2 Malengo Mahususi ya Elimu ya Ualimu

Malengo ya Elimu ya Ualimu ni kumwandaa mwalimu kuwa mahiri katika:

(a) Kukuza uelewa wa kinadharia wa elimu ya ualimu, maadili ya kazi ya ualimu, maadili ya maisha, na misingi ya ualimu;

(b) Kujenga umahiri katika mbinu za kufundishia na kujifunzia;

(c) Kujenga umahiri katika mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia dhana ya ujenzi wa umahiri;

(d) Kukuza ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya mwanafunzi;

(e) Kutumia TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;

(f) Kukuza stadi za utambuzi wa awali wa mwanafunzi mwenye mahitaji maalumu ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;

(g) Kuimarisha matumizi ya lugha katika ufundishaji na ujifunzaji; na

(h) Kujenga stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani*, classroom-based action research*).

## 4.0 Umahiri wa Jumla wa Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu

Umahiri wa jumla umejikita katika misingi ya kuwasiliana, kushirikiana, ubunifu, fikra tunduizi na utatuzi wa matatizo, ujuzi wa kidigiti na uzalendo ambao umefafanuliwa katika maeneo ya ujifunzaji na masomo kama ifuatavyo:

(a) Kutumia nadharia na misingi ya ualimu katika ufundishaji na ujifunzaji;
(b) Kumudu mbinu za kufundishia na kujifunzia;
(c) Kumudu mbinu za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri;
(d) Kumudu mbinu za ubunifu na uvumbuzi katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi;
(e) Kutumia, TEHAMA na teknolojia saidizi katika ufundishaji na ujifunzaji;
(f) Kumtambua mwanafunzi mwenye mahitaji ya ujifunzaji na kutoa afua stahiki;
(g) Kutumia lugha husika kwa ufasaha katika ufundishaji na ujifunzaji;
(h) Kutumia stadi za uongozi katika taaluma (yaani, *instructional leadership*); na
(i) Kumudu stadi zinazolenga kuboresha ufundishaji, ujifunzaji na upimaji (yaani, classroom-based action research).

## 5.0 Umahiri Mkuu na Umahiri Mahususi

Jedwali lifuatalo linaonesha umahiri mkuu na umahiri mahususi unaotarajiwa kujengwa na mwalimu tarajali.

**Jedwali Na 1:** *Umahiri Mkuu na Mahususi wa Mwaka wa Kwanza na wa Pili*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
|---|---|
| 1.0 Kumudu misingi ya upimaji na tathimini katika Elimu ya Awali | 1.1 Kuchambua mbinu za upimaji na tathimini katika Elimu ya Awali kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri.<br>1.2 Kumudu mbinu za kuandaa zana za upimaji wa maendeleo ya ukuaji na ujifunzaji wa mtoto kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi |
| --- | --- |
| 2.0 Kutumia matokeo ya upimaji kutathmini maendeleo ya mtoto | 2.1 Kumudu mbinu za kutoa afua stahiki za kuboresha malezi, ufundishaji na ujifunzaji. |

## 6.0 Majukumu ya Mkufunzi, Mwalimu Tarajali na Mzazi katika Ufundishaji na Ujifunzaji

Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji hutegemea ushirikiano baina ya mkufunzi, mwalimu tarajali na mzazi/mlezi. Majukumu yao ni kama yafuatayo:

### 6.1 Mkufunzi

**Mkufunzi anatarajiwa:**

(a) Kukuza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia ujenzi wa stadi za karne ya 21 kwa kutumia mbinu mbalimbali za uwezeshaji zitakazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji. Baadhi ya mbinu zinazopendekezwa ni zile zinazosaidia kukuza uwezo wa kufikiri, kutafakari, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali ili kutatua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kuandaa mazingira wezeshi ya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na kufaragua zana;

(c) Kutoa malezi kwa haki na usawa kwa kila mwalimu tarajali bila kujali tofauti zao; na

(d) Kubaini mahitaji maalumu ya mwalimu tarajali na kumpatia afua stahiki.

### 6.2 Mwalimu Tarajali

(a) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za mafunzo ndani na nje ya darasa ili kuhakikisha kuwa anajenga umahiri uliokusudiwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo usimamizi wa ujifunzaji na ufundishaji, mbinu za kufundishia na mbinu za upimaji zitakazomwezesha kubaini mafanikio na changamoto ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji;

(b) Kushiriki katika mafunzo endelevu kupitia shule zilizo jirani na chuo kwa lengo la kutafsiri nadharia anazojifunza darasani kwa vitendo. Baadhi ya nadharia hizo ni haiba, maandalizi ya somo, kutumia mbinu za kufundishia, kuandaa na kutumia zana na vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kutathmini wanafunzi;

(c) Kufanya kazi chini ya uangalizi wa walimu wazoefu kwa kipindi cha mwaka mmoja ili kuimarisha umahiri na weledi katika fani ya ualimu;

(d) Kushirikiana na wenzake pamoja na mkufunzi katika mchakato wa ujifunzaji; na

(e) Kuzingatia kanuni na taratibu za chuo.

### 6.3 Mzazi

(a) Kusimamia na kufuatilia mwenendo na maendeleo ya mwalimu tarajali katika ujifunzaji; na

(b) Kumpatia mwalimu tarajali mahitaji muhimu pamoja na vifaa vinavyotumika katika shughuli za ujifunzaji.

## 7.0 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji

Ufundishaji na ujifunzaji wa somJo la Upimaji na Tathmini katika Stashahada ya Ualimu utaongozwa na ujenzi wa umahiri unaotumia mbinu zinazomfanya mwalimu tarajali kuwa kitovu cha ujifunzaji na mkufunzi kuwa mwezeshaji. Mkufunzi atapaswa kutumia mbinu zinazomshirikisha mwalimu tarajali katika tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia umri, mahitaji anuai, na uwezo wake. Mbinu hizo ni ujifunzaji shirikishi unaomwezesha mwalimu tarajali kufikiri, kutafuta maarifa kutoka vyanzo mbalimbali, majadiliano katika vikundi, na kushiriki katika kutoa mrejesho. Njia nyingine ni ziara za kimasomo, kazi za vitendo, na kazi nyingine kama hizo kulingana na muktadha ili kufanikisha ujifunzaji.

## 8.0 Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji

Zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa kuwa shirikishi na zinavyokidhi mahitaji, matakwa na uwezo wa mwalimu tarajali. Mkufunzi anapaswa kuhakikisha mwalimu tarajali anapata nafasi ya kuona, kusikia, na kushika vifaa na zana. Aidha, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinapaswa zimsaidie mwalimu tarajali kuelewa kinachofundishwa. Mkufunzi anashauriwa kutumia zana zinazopatikana katika mazingira yake. Zana hizi zimependekezwa katika Jedwali Na. 3 na 4 la maudhui katika safu ya

zana. Mkufunzi anaweza kutumia zana zaidi ya hizi zinazopendekezwa kulingana na uhitaji ili kufikia lengo la ufundishaji na ujifunzaji.

## 9.0 Upimaji wa Maendeleo ya Ujifunzaji

Upimaji wa maendeleo ya ujifunzaji ni suala muhimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji katika somo la Upimaji na Tathmini Elimu ya Awali ngazi ya Stashahada ya Ualimu. Mkufunzi anapaswa kubuni shughuli nyingi zaidi za upimaji ili kuchochea ujifunzaji.

Katika kuamua kiwango cha ufaulu wa mwalimu tarajali upimaji wa mwisho (tamati) utachangia asilimia sabini (70%) na upimaji endelevu utachangia asilimia thelathini (30%). Mwalimu tarajali anapaswa kufaulu upimaji endelevu kwa angalau asilimia hamsini (50%) na upimaji tamati kwa angalau kiwango hichohicho ili aweze kutunukiwa cheti. Endapo hatafikisha asili mia hamsini (50%), mwalimu tarajali anaweza kurudia mitihani hiyo mara mbili ndani ya miaka mitatu. Jedwali Na. 2 linaonesha mgawanyo wa alama katika upimaji endelevu.

**Jedwali Na. 2:** *Mchanganuo wa Alama za Upimaji Endelevu*

| **Na** | **Shughuli za upimaji** | **Mgawanyo (%)** |
|---|---|---|
| 1 | Mtihani wa Muhula wa Kwanza wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 2 | Mtihani wa Mwisho wa Mwaka wa Kwanza | 6.0 |
| 3 | Mtihani wa Muhula wa Kwanza wa Mwaka wa Pili | 6.0 |
| 4 | Kazi mradi | 7.0 |
| 5 | Mkoba wa Kazi | 5.0 |
| | **Jumla** | **30** |

## 10.0 Idadi ya Vipindi

Muhtasari wa Somo la Upimaji na Tathmini Stashahada ya Ualimu unatoa makadirio ya muda utakaotumika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia uzito wa umahiri mahususi na shughuli za kutendwa na mwanafunzi. Makadirio haya ya muda yamewekwa kwa mfumo wa vipindi ambapo kila kipindi ni dakika 60. Idadi ya vipindi kwa somo hili ni vipindi viwili (2) kwa wiki.

## 11.0 Maudhui ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Maudhui ya ufundishaji na ujifunzaji yamepangiliwa katika jedwali lenye vipengele sita ambavyo ni; umahiri mkuu, umahiri mahususi, shughuli za ujifunzaji, vigezo vya upimaji, zana za ufundishaji na ujifunzaji zinazopendekezwa na idadi ya vipindi. Maudhui hayo yameoneshwa katika Jedwali Na. 3 na 4.

**Jedwali Na 3:** *Maudhui ya Mwaka wa Kwanza*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu misingi ya upimaji na tathmini katika Elimu ya Awali | 1.1 Kuchambua mbinu za upimaji na tathmini katika Elimu ya Awali kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri | (a) Kufafanua dhana za upimaji na tathmini kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri (*maana, aina, madhumuni, sifa, misingi na kuhusianisha nadharia za ujifunzaji na upimaji na tathmini*) | Maana, aina, sifa, madhumuni, misingi na nadharia za upimaji na tathmini zinazotumika kupima na kutathmini watoto wa Elimu ya Awali kwa usahihi zimefafanuliwa | Bango kitita la picha za ukuaji wa mtoto | 40 |
| | | (b) Kuhusianisha ukuaji na ujifunzaji wa mtoto (*domains of child development and learning*) na upimaji na tathmini | Nyanja kuu za ujifunzaji (*domains of learning*) na upimaji na tathmini zake kwa watoto wa elimu ya awali zimehusianishwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (c) Kubainisha mbinu za upimaji na tathmini katika ufundishaji na ujifunzaji wa darasa la awali kwa kuzingatia nyanja kuu za ukuaji na ujifunzaji | Mbinu za upimaji na tathmini katika ufundishaji na ujifunzaji wa darasa la watoto wa Elimu ya Awali kwa kuzingatia nyanja kuu za ukuaji na ujifunzaji zimeanishwa | | |
| | | (d) Kuchambua mbinu za upimaji na tathmini za mtoto zinazozingatia ujenzi wa umahiri katika darasa kubwa | Mbinu za upimaji na tathmini unaozingatia ujenzi wa umahiri kulingana na ukubwa wa darasa la elimu ya awali zimechambuliwa | | |

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| | 1.2 Kumudu mbinu za kuandaa zana za upimaji wa maendeleo ya ukuaji na ujifunzaji wa mtoto kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri | (a) Kuchambua zana za upimaji zinazozingatia ujenzi wa umahiri katika Elimu ya Awali | Zana za upimaji zinazozingatia ujenzi wa umahiri katika makuzi na ujifunzaji wa mtoto wa Elimu ya Awali zimechambuliwa | Chati pindu zenye mada za upimaji na tathmini katika elimu ya awali | 30 |
| | | (b) Kutumia teknolojia katika upimaji na tathmini katika Elimu ya Awali | Matumizi sahihi ya teknolojia katika Upimaji na Tathmini yamebainishwa. | | |

**Jedwali Na 4:** *Maudhui ya Mwaka wa Pili*

| Umahiri mkuu | Umahiri mahususi | Shughuli za ujifunzaji | Vigezo vya upimaji | Zana za Ufundishaji na Ujifunzaji zinazopendekezwa | Idadi ya vipindi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1.0 Kumudu misingi ya upimaji na tathmini katika Elimu ya Awali | 1.1 Kumudu mbinu za kuandaa zana za upimaji wa maendeleo ya ukuaji na ujifunzaji wa mtoto kwa kuzingatia ujenzi wa umahiri | (a) Kumudu uchambuzi wa taarifa za upimaji na tathmini kwa kuzingatia zana za upimaji | Taarifa za upimaji na tathmini kwa kuzingatia zana za upimaji zimechambuliwa | Bango kitita lenye mada ya uchambuzi wa taarifa za upimaji na tathmini | 35 |
| 2.0 Kutumia matokeo ya upimaji kutathmini maendeleo ya mtoto | 2.1 Kumudu mbinu za kutoa afua stahiki za kuboresha malezi, ufundishaji na ujifunzaji | (a) Kutumia matokeo ya upimaji na tathmini katika kuboresha ufundishaji na ujifunzaji | Matokeo ya upimaji na tathmini kwa watoto wa Elimu ya Awali kuboresha ujifunzaji na ukuaji wa mtoto yametumika kama inavyostahili | Ripoti na matini mbalimbali ya ujifunzaji na ukuaji wa watoto wa elimu ya awali | 35 |

**Bibliografia**


James, P. W. (1993). *Educational Evaluation (3rd Ed). Pearson Education Inc.*

Peter, F. O. (2001). *Developing Curriculum (5th Ed), Longman.*

Suc, R. (2012). *Developing Positive Relationship in Schools.Western Sydney and Exeter University College.*

Snow, C. E., & *Van Hemel, S. B. (2008). Early childhood assessment: Why, what, and how. The National Academies Press.*

TET. (2003). *Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti, Moduli ya Somo la Mitaala na Ufundishaji, TET.*

TET. (2003). *Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti, Moduli ya Somo la Upimaji, Tathmini na Utafiti, TET.*

TET. (2013). *Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti Elimu ya Msingi, Moduli ya Kujifunzia Ufundishaji Somo la Ualimu wa Elimu ya Awali. TET.*

TET. (2013). *Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti Elimu ya Msingi; Moduli ya kujifunzia Somo la Ualimu, TET.*

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi [WyEMU]. (2009). *Muhtasari wa Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti Elimu ya Msingi, Somo la Ualimu, WEMU.*

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia [WyEST]. (2014). *Sera ya Elimu na Mafunzo, WEST.*

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia [WyEST]. (2016). *Mtaala na Muhtasari wa Elimu ya Awali. WyEST.*

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia [WyEST]. (2019). *Kiunzi cha Mtaala wa Mafunzo ya Ualimu, WyEST.*

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia [WyEST]. *(2019). Mtaala wa Mafunzo ya Astashahada ya Ualimu, WyEST.*

Wizara ya Elimu na Utamaduni [WyEU]. (2003). *Ualimu Ngazi ya Cheti, Muhtasari wa Somo la Saikolojia na Unasihi, WyEU.*

Wizara ya Elimu na Utamaduni [WyEU]. (2003). *Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti, Muhtasari wa Misingi ya Elimu, WyEU.*